# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS-TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

Kumb.Na:RSS/SEL/2023/01
Mkuu Wa Shule: 0786996117
Makamu Mkuu Wa Shule: 0759792140

Email: raranyasecondary@gmail.com

Shule Ya Sekondari Raranya,
S.L.P 74,
Shirati-Rorya,

**1 Desemba, 2023 .**

Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi…………………………………………………………….
S.L.P……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RARANYA - 2024.**

## 1. UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka **2024**. Muhula wa masomo utaanza tarehe **08/01/2024**.Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024.** Mara mwanafunzi afikapo shuleni aripoti ofisi ya **Makamu Mkuu wa Shule** kwa mapokezi na usajili **ndani ya muda wa kazi**. Makamu Mkuu wa shule atahakikisha kwamba mwanafunzi amekuja na **mahitaji yote** yanayotakiwa.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1. SARE YA SHULE

Sare za shule hii ni **kijani kibichi** na **damu ya mzee.**

#### 2.1.1. WASICHANA

(i) Sketi mbili(2) ndefu (**zinazofika kwenye visigino**), rangi ya **kijani kibichi** na nyingine **damu ya mzee**. Vitambaa vya suruali zitumike kushona sketi (kitambaa namba moja). **Rinda box kubwa 1 mbele na kubwa 1 nyuma na marinda madogo madogo mawili kila upande.**
(ii) Hijabu nyeupe kama ni lazima kwa Waislamu
(i) Soksi **nyeupe ndefu jozi mbili(2)**.

**2.1.2 WAVULANA**

(ii) Suruali mbili(2) moja rangi ya **kijani kibichi** na nyingine **damu ya mzee** (kitambaa namba moja) .(**zisiwe za mtindo wa modal na zisiwe za kubana**) size 16 kwenye miguu pia ziwe na marinda mawili kila upande.
(iii) Soksi jozi mbili (2) **nyeusi**.
(iv) Mkanda mweusi wa kawaida

**2.1.3 KWA WOTE (WASICHANA NA WAVULANA)**

(v) Mashati mawili(2) meupe yenye mikono mifupi (zisiwe za kubana).
(vi) Masweta mawili(2) rangi ya **kijani kibichi** na nyingin**e damu ya mzee .**
(vii) Tai moja rangi ya **kijani kibichi** na nyingin**e damu ya mzee .**
(viii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kufunika miguu na yenye kamba
(ix) T-shirt moja yenye kola rangi ***kijani kibichi***. **Mzazi zingatia rangi hiyo na uwepo wa kola ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza. Aje nayo siku ya kuripoti.**
(x) Bukta moja kwa ajili ya michezo. Rangi ya **nyeusi.**
(xi) **Track suit** rangi **kijani kibichi** kwa ajili ya michezo. Pia track suit hiyo itavaliwa na raba siku ya michezo.
(xii) **Ream paper moja aina ya double A** kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya mwanao hapa shuleni.
(xiii) Madaftari 9 Quire 2, na madaftari madogo 9 kwa ajili English Orientation Course na mazoezi.
(xiv) Mkebe wa hesabu, kalamu na kamusi ya kiingereza.
(xv) Ili kuboresha mazingira ya shule,aje na miche miwili (2) ya miti ya kivuli au matunda. Miche hii ataipanda na kuitunza hapa shuleni.
(xvi) **File moja** ya kutunza kumbukumbu zake

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu,sayansi na teknolojia na ofisi ya rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji wa shule. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara ya kuripoti shuleni.

(i) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
(iii) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira
(iv) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
(v) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(vi) Kutunza mali ya shule
(vii) Kutonyoa kipara
(viii) Lugha ya Kiingereza itatumika kama lugha ya mawasiliano ndani ya shule.

**3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Ubakaji, Uasherati na ushoga
(iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,mirungi na kadhalika
(iv) Kupigana au kupiga
(v) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(vi) Kudharau bendera ya taifa
(vii) Kuoa au kuolewa.
(viii) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(ix) Kukataa adhabu kwa makusudi
(x) Kuwa na **simu ya mkononi**

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SHULE YA SEKONDARI RARANYA**

Meshack Samora Gallus
**Mkuu Wa Shule.**

**VIAMBATANISHO**

**Kiambatanisho A**

**SHULE YA SEKONDARI RARANYA**

**<u>KIAPO (HATI) YA KUKUBALI</u>**

**KIAPO CHA MWANAFUNZI.**

Mimi (Jina la Mwanafunzi)……………………………………………Nakubali Kwa Dhati Kabisa Nafasi Niliyopewa Na Taifa Kujiunga Na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Raranya ilioko Wilayani Rorya Mkoa wa Mara. Naahidi Kufuata Sheria Zote Za Shule Na Taratibu Zote Kama Zilivyotolewa Na Zitakavyotolewa Na Uongozi Wa Shule Ya Sekondari Raranya.

Saini Ya Mwanafunzi……………………………… Tarehe…………………………………

**KIAPO CHA MZAZI/MLEZI**

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)…………………………………………………………..…Ambaye Ni Mzazi/Mlezi Wa Mwanafunzi……….……………………………………Nimeyasoma Masharti Na Sheria Zote Za Shule Ya Sekondari Raranya ilioko wilayani Rorya Mkoa wa Mara Ambako Kijana Wangu Amechaguliwa Kujiunga na kidato cha kwanza. Naahidi Kwamba Nitamhimiza Mwanangu Kufuata Sheria Na Taratibu Zote Za Shule. Aidha Naahidi Kushirikiana Na Uongozi Wa Shule Katika Malezi Bora Ya Mwanangu Ili Baadaye Awe Raia Bora Na Mwema Wa Taifa Letu.Pia naahidi kumkamilishia mahitaji yake yote ya shule.

Saini Ya Mzazi/Mlezi………………………………

Tarehe………………..

Namba ya simu…………………………………………….

.

**Kiambatanisho B**

**SHULE YA SEKONDARI RARANYA**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)**
**(Sharti ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali)**

Full Name (Student)……………………………………………………………………..

Age…………………Height (in cm)…..............Weight (in kgs)………..................................................

1. Blood count………............... (Red and White)..........................................
2. Stool Examination…………………………………………………….......................
3. Urine analysis……………………………………………………………...............
4. Syphilis and other V.D……………………………………………….……………
5. T.B and Leprosy Test………………………………….............................................................
6. Eye Test……………………………….……………………………………………
7. Ear Test……………………….........................................................................
8. Chest Test……………………………………..……………………………………
9. Abdominal Test……………………………………..…………………………..
10. Blood Group (very crucial)……………………......................................
11. Spleen……………………………………………………………………………..
12. Additional information eg Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases (eg Sickle cell anaemia )
    …………………………………………………………………………….……………………........................
    …………………………………………………………………………………………………………………………

I (**Full name**)…………………………………..certify that the above student is **fit/is not fit** to pursue Secondary Education.

Designation……………………………….…………

Station…………………………….………………

Signature……………………

Date…………………………………..………

Rubber Stamp…………………………………………………